FRONTRUNNER 007

# FRONTRUNNER EXAM

## DARASA LA SITA 2021

## KISWAHILI

**6**

**Time: 1 Hour 40 Minutes**

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA A:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika karatasi hii ya maswali.

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati yay ale uliyopewa.***

Ajali ___ 1 ___ zinazotokea nchini zina kinga. Ni ___ 2 ___ ajali itokee pasi na mwenye makosa. Ukilimfulika suala ___ 3 ___ kwa jicho pevu utaona kuwa kinga ya ajali ___ 4 ___. Tuache ___ 5 ___ za kudai kuwa ajali fulani ___ 6 ___ na ndiyo maana ilitokea. ___ 7 ___ madereva ___ 8 ___ hawazingatii sheria za barabarani. ___ 9 ___ wale wanaozingatia hawawasuti ___ 10 ___ wasiozingatia. Wakati wa kulaumiana umepita. Magari _____ 11 ___ mabovu______ 12 ___. Yule atapatikana na _____ 13 _____ barabarani asimlaumu _____ 14 _____ ila yeye mwenyewe. Si wajua ___ 15 ___?

| | A. | B. | C. | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | mingi | nyingi | vingi | mengi |
| 2. | muhali | rahisi | vyema | wepesi |
| 3. | nzima | mzima | zima | kizima |
| 4. | ziko | liko | kiko | iko |
| 5. | fikira | wazo | busara | wazimu |
| 6. | ingezuilika | ingezuiwa | isingezuilika | lisingezuilika |
| 7. | miongoni mwa | Baadhi ya | Kinyume na | Pamoja na |
| 8. | zetu | wetu | wangu | yetu |
| 9. | naye | Nami | Ati | Nao |
| 10. | wenzangu | wenzao | wenzako | wenzetu |
| 11. | yote | zote | lolote | lote |
| 12. | yapigwe marufuku | yapigwe vita | yavutwe | yalaaniwe |
| 13. | shanyingi | karandinga | gari | katara |
| 14. | yoyote | wowote | yeyote | sote |

15. A. mpanda ngazi hushuka
   B. mie nyumba ya udongo sihimili vishindo
   C. msiba wa kujitakia hauna kilio
   D. yote yang'aayo si dhahabu

**Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi**

16. Chagua usemi wa taarifa ulio sahihi wa.
**"Mgonjwa anatibiwa sasa," muuguzi alisema.**
    A. Muuguzi alisema kuwa mgonjwa anatibiwa wakati huo.
    B. Muuguzi alisema kuwa mgonjwa alikuwa akitibiwa wakati huo.
    C. Muuguzi aliuliza iwapo mgonjwa angetibiwa wakati huo.
    D. Muuguzi alisema mgonjwa anatibiwa sasa.

17. Eleza matumizi ya kiambishi "ji" katika sentensi ifuatayo: **Nilijiuliza maswali mengi kuhusiana na maisha yangu.**
    A. Kuonyesha nafsi
    B. Kuonyesha hali
    C. Kuonyesha ukubwa
    D. Kuonyesha mtendaji

18. Chagua jibu lenye vyombo vya usafiri majini pekee
    A. Purtangi, nchoro, pantoni
    B. Rukwama, shangingi, daladala
    C. Ngalawa, chelezo, dau
    D. Kiberenge, nyambizi, manowari

19. Andika kinyume cha; Baada ya sherehe, wageni walitawanyika
    A. Baada ya sherehe, wageni walijumuika
    B. Kabla ya sherehe, wenyeji walijumuika
    C. Kabla ya sherehe, wageni walijumuika
    D. Baada ya sherehe, wenyeji walijumuika

20. 'Si vizuri kumdharau mtu kwa kumtazama tu, huenda akafanya makuu usiyoamini.' Ni methali gani inayofaa maelezo haya?
    A. Heri jirani kuliko ndugu wa mbali
    B. Mkulima halaumu jembe lake
    C. Mcheka kilema huzaa kilema
    D. Usione wembamba wa reli, garimoshi hupita

21. Chagua kivumishi katika sentensi ifuatayo;
**Wanafunzi watatu walifika shuleni mapema.**
    A. watatu    B. wanafunzi
    C. mapema    D. walifika

22. Wingi wa; Ananipenda nami ninampenda, ni
    A. Wananipenda nasi tunampenda
    B. Wanatupenda nasi tunawapenda
    C. Ninawapenda nao wananipenda
    D. Tunawapenda nao wanatupenda

23. Sentensi gani sahihi kisarufi?
    A. Shoka limekata mti.
    B. Pua limevuja damu.
    C. Zulia imetandikwa sakafuni.
    D. Jua imechomoza.

24. Chagua sentensi iliyotumia tashbihi
    A. Nguo ya mhubiri huyo ni theluji
    B. Mwanamke Yule alilewa chakari baada ya kunywa pombe
    C. Usipooga utanuka mithili ya beberu
    D. Mwizi alipiga mbio alipowaona askari

25. Akisami hii kwa maneno ni, $^{6}/_{8}$
    A. Thumuni sita    B. Thuluthi sita
    C. Sudusi nane    D. Tusui nane

26. Jawabu gani linaloonyesha nomino iliyoundwa kutokana na sifa?

| | **Sifa** | **Nomino** |
|---|---|---|
| A. | Pika | Mpishi |
| B. | Chafu | Mchafu |
| C. | Pana | Upana |
| D. | Safari | Usafiri |

27. Kitendawili "Nikitembea yuko, nikikimbia yuko, nikiingia ndani hayuko," jibu lake ni
    A. Mwangaza    B. Kivuli
    C. Mwangwi    D. Upepo

28. Mtoto wa ndugu yako utamwita _____
    A. Mpwa    B. Mkoi
    C. Binamu    D. Mjukuu

29. Kipindi cha miaka kumi huitwa _____
    A. karne    B. juma
    C. mwongo    D. mwezi

30. Irabu za alfabeti ya Kiswahili ni _____ kwa jumla.
    A. 10    B. 25    C. 30    D. 5

***Soma habari kisha ujibu maswali 31 - 40***

Vita vilikuweko tangu miaka ya zamani. Watu walipigana kwa sababu mbalimbali. Pengine walikuwa wakitetea mali yao. Kuna waliopigana kwa sababu ya kutaka kuonyesha nguvu zao.

Katika vita hivyo vya zamani, silaha zilizokuwa zikitumika sana ni kama mishale na uta, mikuki, ngao na hata panga. Baadaye kukaundwa silaha hatari zaidi. Chache zinaweza kuangamiza miji hata na nchi.

Vita havina faida bali hasara tupu. Madaraja huvunjwa, majumba hubomolewa, mashamba humalizwa na roho hupotezwa. Vita vikimalizika basi akina mama na watoto ndio wanaohangaika zaidi. Hupatikana wajane na mayatima kwa wingi kupita kiasi. Kwa nini basi matatizo hayamalizwi kwa njia ya mazungumzona majadiliano? Kwa nini kuwakosesha watoto nafasi ya kusoma kwa sababu ya vita?

Msumbiji, Sudan, Liberia, Zaire na Rwanda ni kati ya nchi zilizopoteza miaka mingi katika vita.

31. Neno gani lina maana kinyume cha vita?
   A. Manowari
   B. Mchezo
   C. Kicheko
   D. Amani

32. Katika vita vya zamani, silaha zilizokuwa zikitumika sana si kama ___
   A. Mishale na uta
   B. Mikuki na ngao
   C. Makombora na manowari
   D. Panga na mikuki

33. Silaha za kisasa zilizotajwa ni ngapi?
   A. Tatu
   B. Mbili
   C. Nne
   D. Nane

34. Neno gani lina maana ya: Mtoto ambaye wazazi wake wamefariki?
   A. Mjane
   B. Yatima
   C. Maiti
   D. Mauti

35. Ni nani wanaopata taabu zaidi baada ya vita?
   A. Akina mama na wazee
   B. Kina baba na watoto
   C. Akina mama na watoto
   D. Hatujaambiwa

36. Nchi ngapi zimetajwa kuwa zimepigana kwa muda mrefu?
   A. Tatu
   B. Sita
   C. Nne
   D. Tano

37. Vita vilikuweko tangu lini?
   A. Zamani
   B. Juzi
   C. Mwaka uliopita
   D. Samani

38. Ni kweli kusema kwamba ___
   A. Vita havina faida
   B. Vita vina faida
   C. Vita ni nguvu
   D. Vita ni vitamu

39. Kulingana na kisa hiki ___
   A. Vita ni njia ya mazungumzo na majadiliano
   B. Vita huleta manufaa
   C. Baada ya vita hupatikana wajane na mayatima kwa wingi
   D. Vita huleta maendeleo

40. Hadithi hii inatufunza ___
   A. Dawa ya moto ni moto
   B. Vita havina macho
   C. Mwenye macho haambiwi tazama
   D. Mwenye nguvu mpishe

***Read the passage below and answer questions 41 - 50***

Matatu ni jina linalotumiwa kwa magari madogo ya kuwasafirisha abiria. Jina halisi linalofaa kuitwa magari haya ni matwana. Lakini kwa vile nauli ya magari hayo ilikuwa mapeni matatu yalipoanza, jina likafifia. Jina jingine maarufu la matatu ni daladala.

Magari ya matatu yana faida zake na hasara. Watu wengi katika miji mikubwa kama vile Nairobi, Mombasa, Kisumu na miji mingine, huyatumia kusafiria. Huwawezesha kwenda kazini asubuhi na kurudi nyumbani jioni. Watu wengi huyapenda matatu kwa sababu husafiri haraka na wanapoyatumia hawachelewi kufika kazini. Tena huwashukishia karibu na maskani yao badala ya kuwapeleka katika vituo maalum. Kwa matatu, popote ni kituo.

Watu wanaosimamia matatu hujipatia pesa chungu nzima kwani ni biashara kubwa. Madereva na utingo wa magari haya huweza kijipatia pesa za kuyaendesha maisha. Lakini magari haya yana **ila** zake.

Mara nyingi magari ya matatu huendeshwa na madereva ambao hawana leseni za kuendesha magari. Kwa hivyo husababisha ajali nyingi ambazo huwauwa watu wengi. Isitoshe, matatu hujaza watu sana na kuwafanya abiria wakose hewa safi. Baadhi ya magari ya matatu ni makuukuu na huwa ni hatari kwa maisha ya wasafiri.

Kwa sababu ya ila hizi, serikali imeanza mpango wa kuyasaka matatu ambayo hayafuati taratibu zilizowekwa. Madereva wa matatu wanaokosa kufuata sheria za barabarani huchukuliwa hatua kali. Ni vyema sisi sote kama wananchi wazalendo tuiunge serikali mkono ili maisha ya abiria yasiwe hatarini.

41. Jina maarufu la matatu ni ______
    A. Matwana B. Daladala
    C. Matatu D. Basi

42. Malipo ya usafiri kwa matatu ni ______
    A. pesa B. nauli
    C. kivuko D. koto

43. Magari ya matatu
    A. hayana manufaa kwa watu
    B. yana hasara na faida
    C. huwafaa walioyanunua pekee
    D. yana faida pekee

44. Watu wengi huyapenda matatu kwa sababu______
    A. huwawezesha kushukia karibu na kwao
    B. huwa na muziki ndani
    C. hujaa upesi
    D. hayasababishi ajali

45. Kwa sababu ya kubeba watu wengi magari ya matatu huwafanya abiria__________
    A. wafurahi B. watete
    C. wakose hewa safi D. wayapende

46. Magari mengi ya matatu ni__________
    A. mapya
    B. makuukuu
    C. makubwa
    D. ya kuwafurahisha wasafiri

47. Hatari kubwa ya magari ya matatu ni________
    A. husababisha ajali
    B. kuwaibia abiria
    C. kuwapeleka abiria mbio
    D. kuwapeleka abiria safari ndefu

48. Neno jingine lenye maana sawa na ila ni_______
    A. taabu B. shida
    C. uzuri D. kasoro

49. Msaidizi wa dereva katika matatu ni _______
    A. abiria B. tajiri
    C. utingo D. leseni

50. Kichwa kifaacho taarifa hii ni______
    A. Magari B. Usafiri
    C. Mawasiliano D. Matwana